JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI MHESHIMIWA ABDALLAH OMARI KIGODA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2001 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MUDA WA KATI NA MFUMO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2002/03 – 2004/05

Kimetolewa na Ofisi ya Rais Mipango na
Ubinafsishaji, Dar es Salaam, Tanzania

13 Juni, 2002

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2001 na Mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2002/03 – 2004/05. Pamoja na hotuba hii nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2001 na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2002/2003.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa Kamati ya Bunge ya Uchumi na Fedha ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Njelu Kasaka Mbunge wa Chunya kwa mchango mkubwa iliotoa wakati ikijadili muhtasari wa Hotuba hii ambao umetuwezesha kuboresha kazi yetu.

   Aidha, nachukua nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Prof. Joshua Doriye, kwa kazi nzuri ya kufanikisha utayarishaji wa Taarifa hii na mapendekezo ya Mpango ninaouwasilisha leo.

3. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha mwaka mmoja Wabunge wawili walifariki dunia. Wabunge hao ni Marehemu Sebastian Kinyondo (CCM) aliyekuwa Mbunge wa Bukoba Vijijini na Marehemu John Mangwangwa (CCM) aliyekuwa Mbunge wa Mpanda Magharibi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

   Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (CUF) kwa kuteuliwa kuwa Mbunge.

MAPITIO YA MALENGO YA JUMLA YA UCHUMI

4. **Mheshimiwa Spika,** malengo ya jumla ya uchumi yaliyowekwa kwa mwaka 2001/2002 yalikuwa kama ifuatavyo:-
   - Kukuza uchumi kwa kiwango cha asilimia 5.5 mwaka 2001, hadi asilimia 6.2 mwaka 2002 na asilimia 6.3 mwaka 2003;
   - Kupunguza kasi ya upandaji wa bei hadi kufikia kiwango cha asilimia 4.5 mwishoni mwa mwezi Juni 2002;

- Kuongeza mapato ya ndani ya Serikali hadi kufikia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa;
- Kuongeza ujazi wa fedha kwa tafsiri pana kwa viwango vinavyowiana na malengo ya kukuza uchumi na kupunguza kasi ya upandaji wa bei; na
- Kuongeza akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji bidhaa na huduma toka nje kwa zaidi ya miezi minne;

Ukuaji wa Uchumi

5. **Mheshimiwa Spika,** ukuaji halisi wa uchumi ulifikia asilimia 5.6 mwaka 2001 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2000 ukiwa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za kilimo, bidhaa za viwanda, uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli (ikijumuisha utalii), mawasiliano na uchukuzi. Sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2001 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2000. Mchango mkubwa katika sekta ya kilimo umetokana na ongezeko katika uzalishaji wa mazao (hasa ya chakula) uliofikia asilimia 5.9 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2.9 katika mwaka 2000. Sekta ya uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli (ikijumuisha utalii) ilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 6.5 ambapo sekta ya bidhaa za viwandani ilikua kwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na asilimia 4.8 na sekta ya mawasiliano na uchukuzi ilikua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 6.1 katika kipindi hicho.

6. **Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa uchumi unatokana na ongezeko la uzalishaji na utoaji huduma katika sekta mbali mbali za uchumi na linapimwa kwa kutumia vigezo vya uchumi jumla hususan, Pato la Taifa na wastani wa kipato cha mwananchi. Ili nchi iendelee lazima pawepo na ukuaji wa uchumi, lakini vile vile kuwepo na sera za makusudi za kusambaza ukuaji wa uchumi ili maendeleo ya kiuchumi yaweze kuwafikia wananchi walio wengi. Inatia moyo kuona kwamba uchumi wa nchi yetu kwa hivi sasa unakua, kazi iliyoko mbele yetu ni kuweka mkazo katika utekelezaji wa sera na mikakati ya kusambaza matokeo hayo ili kuweza kuboresha maisha ya wananchi wengi zaidi.

Kasi ya Upandaji Bei

7. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2001/02, kasi ya upandaji bei iliendelea kushuka kutoka asilimia 5.1 Julai 2001 hadi asilimia 4.6 Mei 2002 na matarajio ni asilimia 4.5 ifikapo Juni 2002. Mwenendo huu mzuri wa kushuka kwa kasi ya upandaji bei umechangiwa na upatikanaji na usambazaji wa chakula; udhibiti wa matumizi ya serikali ikiwa ni pamoja na udhibiti wa ujazi wa

fedha; na kuboreshwa kwa shughuli za mawasiliano na uchukuzi baada ya kukarabati miundombinu mbalimbali.

8. **Mheshimiwa Spika**, kasi ya upandaji bei imeendelea kupungua kutoka asilimia 30 mwezi Desemba, mwaka 1995 hadi asilimia 4.6 mwezi Mei 2002, lakini wananchi wengi hawajafaidika kutokana na kupungua kwa kasi ya upandaji bei kutokana na uwezo wao kuwa mdogo kifedha. Uwezo wa wananchi kifedha kumudu kununua bidhaa umeendelea kuwa mdogo kutokana na kutokuwepo ongezeko linaloridhisha la pato halisi (disposable income) kwa wananchi walio wengi. Uchumi wetu ungetengemaa zaidi kama kushuka kwa kasi ya upandaji bei kungetokana pia na kuongezeka kwa huduma na uzalishaji wa bidhaa zinazotumiwa nchini.

Mapato na Matumizi ya Serikali

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2001/02 mapato ya ndani yalikisiwa kufikia asilimia 12.1 ya pato la taifa, ambapo uwiano wa matumizi ulitarajiwa kufikia asilimia 21.1. Takwimu tulizonazo zinaonyesha kwamba hadi kufikia Juni 2002 mapato ya ndani ya serikali yatafikia asilimia 12.2 na matumizi yanatarajiwa kufikia asilimia 21.1. Uwiano wa mapato ya ndani kwa pato la taifa bado ni mdogo ikilinganishwa na nchi jirani. Hii inatokana na sababu kuu tatu. Kwanza, asilimia kubwa ya uchumi wetu unategemea uzalishaji katika sekta ya kilimo, ambayo ina wigo mdogo ambao kwa sehemu kubwa bado uko nje ya mfumo wa kutoza kodi. Pili, sekta isiyo rasmi (informal sector) ambayo huchangia asilimia 30 ya pato la taifa bado haijajumuishwa katika mfumo rasmi wa kuwezesha washiriki wake kulipa kodi. Tatu, idadi ya watu wanaolipa kodi ya mapato na ya VAT ni ndogo sana. Kama sote tutashiriki kikamilifu kuhamasisha watu wengi zaidi walipe kodi nina hakika tunaweza kuongeza uwiano wa mapato yetu kwa pato la taifa, kufikia angalau asilimia 15.

Karadha na Ujazi wa Fedha

10. **Mheshimiwa Spika**, ujazi wa fedha kwa maana pana (M_2), uliongezeka kwa asilimia 12.2 katika kipindi cha Juni-Desemba 2001, juu kidogo ya lengo la asilimia 12. Aidha, viwango vya riba kwa mikopo toka mabenki ya biashara viliendelea kuwa juu sana kufikia asilimia 20, wakati riba inayotolewa kwa amana katika mabenki hayo imeendelea kushuka kwa wastani wa asilimia 3 hadi 5, hata baada ya mfumuko wa bei kushuka kwa kiwango kikubwa. Hali hii imefanya wawekezaji wengi kushindwa kutumia huduma za mikopo kutoka

katika mabenki hayo, na kwa sababu hiyo, mchango wa mabenki hayo katika ukuaji wa uchumi bado uko chini kuliko uwezo wake.

11. **Mheshimiwa Spika,** mabenki hayo pia yameendelea kupendelea kuwekeza zaidi katika hawala za serikali. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na mabenki hayo kutoona ulazima wa kukopesha sekta binafsi kama njia muhimu ya mapato yao. Azma ya serikali ni kuendeleza udhibiti wa ujazi wa fedha ili utengamano wa uchumi uliopo uweze kuwa endelevu na kuyafanya mabenki kutoa mikopo kwa riba za kadri.

Mauzo na Uagizaji Bidhaa Nje

12. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya mauzo ya bidhaa nchi za nje iliongezeka kwa asilimia 17 kutoka dola 663.2 milioni mwaka 2000 hadi dola 776.4 milioni mwaka 2001. Bidhaa zisizo asilia ndizo zimekuwa chanzo kikubwa cha ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa nje. Mchango wake uliongezeka kutoka asilimia 55.8 mwaka 2000 hadi asilimia 70.1 mwaka 2001 na kufanya nafasi ya bidhaa asilia kushuka sawia kutoka asilimia 44.2 hadi asilimia 29.9. Kushuka huko kulisababishwa na kushuka kwa bei ya bidhaa hizo katika soko la dunia, kupungua kwa uzalishaji, ubora na uhafifu wa baadhi ya bidhaa zetu; na uwezo mdogo wa kuhimili ushindani katika masoko ya nje. Vile vile, uagizaji wa bidhaa toka nje uliongezeka kutoka dola 1,334.9 milioni mwaka 2000 hadi dola 1,489.7 milioni mwaka 2001.

13. **Mheshimiwa Spika,** kama takwimu hizi zinavyoonyesha, pengo la thamani ya bidhaa zinazouzwa nje na zile tunazoagiza toka nje ni kubwa. Hii ni kwa sababu kubwa mbili: Mosi, biashara yetu ya nje imekita sana katika mazao ya asilia ambayo thamani yake katika Soko la dunia imezidi kupungua mwaka hadi mwaka. Pili, sehemu kubwa ya bidhaa tunazoagiza nje ni za viwandani kama vile mitambo na mashine; mafuta na malighafi nyingine za viwandani, ambazo hatuwezi kuepuka kuagiza ili kukidhi mahitaji ya nchi kuendeleza uzalishaji wa ndani.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika kurekebisha hali hii isiyoridhisha ya urari wa biashara ya nje, serikali kwa upande wake imeendelea na jitihada za kukuza mauzo nje kwa kufanya yafuatayo: kuweka taratibu na kupitisha sheria ya uanzishwaji wa maeneo huru ya uwekezaji na usindikaji wa bidhaa za kuuza nje, kuweka mfumo rasmi wa mashauriano kati yake na sekta binafsi kupitia

Baraza la Taifa la Biashara, kuingia mikataba mbali mbali ya kimataifa inayowapa fursa wafanya biashara kuuza bidhaa zao nje bila vikwazo kama vile mikataba ya AGOA na Coutonou na kushirikisha sekta binafsi katika safari za nje za maonyesho ya kibiashara na hata zile za mashauriano ya kiserikali.

Akiba ya Fedha za Kigeni

15. **Mheshimiwa Spika**, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 18.7 kutoka dola 974.4 milioni mwaka 2000 hadi dola 1,156.6 milioni mwaka 2001 kiasi ambacho kinatosheleza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa muda wa miezi 6.1, ikiwa ni zaidi ya lengo la miezi 4.0. Ongezeko hili lilichangiwa na kuimarika kwa shughuli za wawekezaji wa nje, misaada toka kwa wahisani, mapato yatokanayo na utalii na ununuzi wa fedha za kigeni unaofanywa na Benki Kuu (InterBank Foreign Exchange Market-IFEM).

UWEKEZAJI NA UKUZAJI RASILIMALI

Ukuaji wa Sekta Binafsi

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Januari – Desemba 2001, jumla ya miradi 163 yenye thamani ya sh. 1,091,805 milioni iliidhinishwa na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC), ikilinganishwa na miradi 178 yenye thamani ya sh. 699,771 milioni iliyoidhinishwa mwaka 2000. Sekta zilizovutia wawekezaji zaidi ni uzalishaji bidhaa za viwandani, ambayo imewekeza asilimia 46 ya miradi yote; uuzaji jumla, rejareja na mahoteli (inayojumuisha utalii) asilimia 14; kilimo na mifugo asilimia 7.5. Ili kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji wa nje, TIC ilitembelea nchi za Ulaya na Asia: kama vile Ufaransa, Malaysia, Japan, India na Pakistan ili kunadi miradi ya kuwekeza.

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2001/02, serikali imeanzisha Baraza la Taifa la Biashara kama kiungo muhimu cha kukuza mashauriano na sekta binafsi kuhusu masuala ya sera na sheria za uwekezaji yanayolenga katika kujenga uchumi imara na kuleta maendeleo endelevu nchini. Katika kipindi hiki, pia Serikali imeendelea kutekeleza programu maalumu inayolenga katika kuweka mazingira bora ya uendeshaji biashara nchini (Business Environment Strenghthening for Tanzania – BEST) na hivyo kupunguza urasimu, kuimarisha vivutio vikiwemo vile vinavyotolewa na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji Rasilimali.

18. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi za kuongeza uwekezaji rasilimali nchini bado uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa ni mdogo ikilinganishwa na miaka ya 1990 ambapo sehemu kubwa ya uwekezaji ilikuwa mikononi mwa serikali na mashirika yake. Kwa mfano, mwaka 2001 uwiano huo ulikuwa asilimia 20.4 ikilinganishwa na kiwango cha juu kilichowahi kufikiwa cha asilimia 30 mwaka 1991. Bado Sekta Binafsi inachangamoto la kuziba pengo hilo.

HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIUCHUMI KIMATAIFA:

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa jumla hali ya uchumi duniani haikuwa nzuri mwaka 2001. Pato la dunia liliongezeka kwa asilimia 2.4 mwaka 2001 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.7 mwaka 2000. Kwa upande wa nchi zilizoendelea, pato lao lilikua kwa asilimia 1.1 mwaka 2001 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2000. Pato la nchi zinazoendelea lilikua kwa asilimia 4.0 mwaka 2001 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2000. Pato la Afrika lilikua kwa asilimia 3.5 mwaka 2001 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2000. Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, pato lilikua kwa wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2001 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2000.

20. **Mheshimiwa Spika**, kudhoofu kwa uchumi wa dunia kumetokana hasa na kuyumba kwa uchumi wa nchi zenye viwanda vingi duniani zikiongozwa na Marekani. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ulipungua kufuatia kuendelea kwa migogoro ya wenyewe kwa wenyewe, kushuka kwa bei za bidhaa asilia katika soko la dunia, ukame, na kuenea kwa athari za ugonjwa wa ukimwi.

BIASHARA NA JUMUIYA ZA USHIRIKIANO

Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki (EAC)

21. **Mheshimiwa Spika**, nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zimeendelea na juhudi zake za kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Juhudi za kukamilisha maandalizi ya itifaki ya ushuru wa pamoja wa forodha (Customs Union) ziliendelea. Maeneo muhimu ambayo yatazingatiwa katika itifaki ya ushuru wa pamoja wa forodha ni:- Uondoaji wa ushuru wa bidhaa kwa biashara ndani ya Jumuiya (Elimination of Internal Tariff); Uanzishaji wa mfumo mmoja wa ushuru wa forodha (Common External Tariff); Utaratibu wa kuhakiki uasili wa bidhaa (Rules of Origin).

22. **Mheshimiwa Spika**, itifaki ya ushuru wa pamoja wa forodha inatakiwa iwe tayari ifikapo Juni, 2004 au mapema. Aidha, Jumuiya imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo kwa kuendeleza miradi ya ushirikiano kwenye kilimo na usalama wa chakula, nishati, utalii, usalama wa anga, hali ya hewa, posta, ushirikiano wa vyuo vikuu na hifadhi ya mazingira kwenye bonde la Ziwa Victoria.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (Southern African Development Community – SADC):

23. **Mheshimiwa Spika**, nchi wanachama zilitakiwa kuunda Kamati za Taifa kuratibu utekelezaji wa sera, mikakati na programu za jumuiya katika nchi hizo. Tanzania imekwishaunda kamati yake. Katika kipindi cha mwaka 2001, Tanzania iliridhia itifaki kadhaa. Chini ya itifaki ya biashara nchi wanachama zimekubali kushirikiana kwa kuondoa ushuru wa biashara; kuweka utaratibu wa kuthibiti uasili wa bidhaa (Rules of Origin); na kulegeza masharti ya biashara ya huduma. Lengo ni kuondoa vikwazo visivyo vya ushuru (non-tariff barriers to trade) na kuondoa ushuru wa bidhaa za kawaida katika kipindi cha miaka 8 hadi 12 kwa bidhaa nyeti.

Shirika la Kimataifa la Biashara (WTO)

24. **Mheshimiwa Spika,** kama waheshimiwa wabunge wanavyofahamu, biashara baina ya mataifa inasimamiwa na Shirika la Kimataifa la Biashara (WTO). Nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania ziko katika hali ngumu katika kutekeleza masharti ya shirika hilo kutokana na uchanga wa nchi hizo katika masuala

mbalimbali ya kimsingi kama vile teknolojia duni, ukosefu wa viwanda vya kisasa na uwezo mdogo wa kiufundi katika masuala ya biashara.

25. **Mheshimiwa Spika,** ili kukabili baadhi ya mapungufu hayo, nchi maskini sana duniani zilifanya mkutano Zanzibar ili kujiwekea msimamo wa pamoja katika masuala ya WTO na hasa katika mkutano wa kawaida uliofanyika huko Doha, Qatar Novemba, 2001. Katika mambo yaliyojadiliwa, ilikubalika nchi tajiri kuondoa ruzuku zinazowekwa kwenye bidhaa za kilimo zinazosafirishwa nje, sambamba na kupunguza ushuru unaotozwa kwa bidhaa kutoka nchi maskini sana. Vile vile, nchi wanachama ziliafikiana kuwa makubaliano yaliyofikiwa kuhusu hatimiliki yasizuie nchi hizo kuchukua hatua za kulinda afya za raia wao. Makubaliano mengine ni haki ya nchi mwanachama kutoa leseni ya kutengeneza au kununua dawa kwa bei nafuu zisizo na hatimiliki ili kuokoa maisha ya raia wake. Nchi zilizoendelea ziliahidi pia kutoa misaada ya kujenga uwezo wa nchi maskini kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya shirika hilo.

UREKEBISHAJI NA UBINAFSISHAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

26. **Mheshimiwa Spika,** hadi sasa idadi ya mashirika ambayo yamekwishabinafsishwa ni 257 au asilimia 70 ya jumla ya mashirika yote. Thamani ya mikataba yote ni sh. 75.8 bilioni na dola za marekani 378.3 milioni. Serikali imekwishapokea malipo ya sh. 44.02 bilioni na US $ 187.7 milioni. Kwa hivi sasa PSRC imebakiza mashirika 69 na “entities” nyingine 52 ambazo zipo katika hatua mbali mbali za ukodishaji/ubinafsishaji. Mashirika yaliyopo kwenye hatua ya makubaliano ya awali yana thamani ya mikataba ya sh. 5.5 bilioni na US $ 22.03 milioni. Kiasi kilichopatikana ni sh. 1.43 bilioni na US $ 1.9 milioni na malipo mengine yanangojea kukamilisha majadiliano na wawekezaji. Uuzaji wa mali nyinginezo za mashirika (*non core assets)* umeingizia Serikali mapato ya sh. 8.2 bilioni na US $ 185,000. Malimbikizo ya madeni kwa mashirika/makampuni yaliyobinafsishwa ni shs. 4.8 bilioni na US $ 5.1 milioni. PSRC imefanikiwa kukusanya kiasi cha shs. 239.5 milioni na US $ 544,681.

27. **Mheshimiwa Spika,** hivi sasa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) imeendelea na urekebishaji na ukodishaji wa mashirika makubwa yanayotoa huduma muhimu kwa wananchi kama vile DAWASA, TRC, TANESCO, NIC NA NMB.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika jumla ya mashirika 257 yaliyobinafsishwa hadi sasa, 122 yamepata wawekezaji/wanunuzi Watanzania kwa asilimia 100; mashirika 14 yamepata wawekezaji wa nje kwa asilimia 100 na mashirika 190 yaliyobaki yamebinafsishwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali, wawekezaji wa nje na wawekezaji wa ndani. Kati ya mashirika yaliyobinafsishwa kwa Watanzania, kumi yamechukuliwa na wafanyakazi wa mashirika au Kampuni zinazohusika. Mashirika hayo ni:- Tanzania Publishing House, TISCO, NEDCO, KIUTA, National Steel Corporation, HANDICO, Express (T) Limited, Moshi Hand Tool Limited, Shirika la Usafirishaji la Taifa (NTC) na Arusha Metal Industries Limited.

Aidha, kwa mwaka 2001/02, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) imebinafsisha jumla ya mashirika 15 kati ya lengo la mashirika 40 na mali nyingine za mashirika hayo.

29. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kusisitiza kwamba sera ya serikali katika kubinafsisha mashirika ya umma ya miundombinu muhimu yanayotoa huduma kwa wananchi walio wengi ni kukodisha na sio uuzaji wa moja kwa moja. Hii ndiyo sera ya serikali, na ndiyo itakayotumika katika ubinafsishaji wa mashirika makubwa ya miundombinu kama vile TANESCO, TRC na kadhalika.

30. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu mashamba makubwa ya kilimo na mifugo na ranchi za taifa, napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba serikali imekwishafanya uamuzi wa kuanza kuyabinafsisha. Katika kutekeleza azma hii kipaumbele kitawekwa katika kuwapa maeneo wakulima wadogo wadogo hasa kwenye yale maeneo yenye uhaba wa ardhi. Utaratibu wa ubinafsishaji wa mashamba haya utasaidia kuendeleza matumizi ya ardhi yetu ambayo imekaa kwa muda mrefu bila ya kuzalisha.

31. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji umeleta mafanikio. Kwa mfano, viwanda ambavyo havikuwa vinalipa kodi kabla ya kubinafsishwa sasa vimeanza kulipa kodi. Kiwanda cha Karatasi cha Kibo kililipa kodi ya shilingi 460 milioni mwaka 1999 ikilinganishwa na shilingi 662.00 milioni mwaka 2000, Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kililipa dola 2.0 milioni mwaka 1998 ikilinganishwa na dola 6.9 milioni mwaka 2000 na Kiwanda cha Maturubai

Morogoro kililipa shilingi 145 milioni mwaka 1998 ikilinganishwa na shilingi 800 milioni mwaka 2000. Ufanisi katika uzalishaji na utoaji huduma umeongezeka kama uzalishaji wa sukari kutoka tani 113,622 mwaka 1998/9 hadi kufikia tani 164,500 mwaka 2001/02 na kitengo cha makontena kimepunguza siku za kuondoa mizigo bandarini kutoka siku 44 hadi siku 11. Zaidi ya asilimia 75 ya mashirika yaliyobinafsishwa yameanza kufanya kazi. Serikali inayafuatilia mashirika machache ambayo hayaendeshwi vizuri tangu yabinafsishwe ili kubaini matatizo yaliyojitokeza kwa lengo la kuchukua hatua zinazofaa kulingana na mikataba iliyosainiwa na wawekezaji hao.

32. **Mheshimiwa Spika,** hata hivyo bado kuna matatizo yanayoendelea kulikumba zoezi la ubinafsishaji kama vile wadaiwa sugu, wazabuni wasiokuwa na uwezo na uaminifu, kutofahamu na hivyo kutoridhika na umuhimu wa ubinafsishaji na uwezo mdogo wa ufuatiliaji. Serikali imechukua hatua kadhaa kutatua matatizo haya, nazo ni pamoja na kuajiri wakusanyaji madeni, kuhakiki undani na wasifu wa wazabuni; kuanzisha utaratibu wa kuambatanisha 'bid bond' ya asilimia tano, kuendesha warsha za viongozi na wadau na kuanzisha vitengo vya ufuatiliaji kwenye Wizara mbalimbali.

UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO 2025

33. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya hadi 2025 ulianza kwa kurekebisha sheria na kanuni zinazoongoza uchumi, kutayarisha na kuhuisha sera, mikakati na programu mbali mbali za maendeleo. Kwa mfano, Bunge limerekebisha sheria ya uwekezaji rasilimali ya mwaka 1997, sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 na kupitisha sheria ya kuanzishwa kwa maeneo maalum ya usindikaji wa bidhaa za kuuza nje. Aidha, kati ya mwaka 1998 na 2002, serikali imebuni sera ya mikopo midogo, sera ya taifa ya maendeleo ya wanawake, mpango wa kuboresha sekta ya elimu; mpango wa maendeleo ya barabara, na mkakati wa taifa wa kuzuia maambukizi ya ukimwi; vyenye lengo la kurahisisha utekelezaji wa Dira.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2001/02 serikali ilisimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo kwa: Kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupunguza umasikini nchini, kujenga mfumo mzuri wa fedha utakaowezesha wawekezaji wa ndani kupata mikopo ili kuwawezesha kuwekeza katika sekta za uzalishaji mali; kutayarisha mikakati ya kuendeleza sekta ya kilimo na maendeleo vijijini ambayo inalenga katika kutekeleza malengo ya muda mrefu ya Dira na kuimarisha utawala bora ili kurahisisha ushiriki wa wananachi katika maendeleo yao.

Aidha, wataalam wameendelea kufanya uchambuzi wa kina kwa lengo la kuweka malengo ya muda wa kati na kuyaainisha ili yawe na mwingiliano na malengo ya mikakati na programu mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa nchini. Katika ngazi ya Mikoa na Wilaya wataalamu waliendelea kukamilisha zoezi la kuchambua fursa zilizopo na kubaini vikwazo ili kurahisisha utayarishaji wa mipango ya maendeleo ya kutekeleza Dira ya Maendeleo.

SEKTA ZA UZALISHAJI MALI

Sekta ya Kilimo

35. **Mheshimiwa Spika**, sekta hii ilikua kwa wastani wa asilimia 5.5 ukilinganisha na asilimia 3.4 kwa mwaka 2000. Ukuaji huu ni matokeo ya jitihada kubwa zilizofanywa na wakulima vijijini, serikali kutengemaza uchumi unaoendana na utekelezaji wa sera za jumla za kiuchumi pamoja na misaada inayotolewa na wahisani mbalimbali katika sekta ya kilimo. Vile vile, ushiriki wa sekta binafsi na hali nzuri ya hewa hasa upatikanaji wa mvua za kutosha kwa maeneo yaliyo mengi nako kulichangia katika ongezeko hili.

36. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2001/02, serikali iliendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo katika masuala yafuatayo:-

- Utayarishaji wa Mkakati wa miaka 5 wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na kukamilisha maandalizi ya Programu ya utekelezaji ambapo programu ndogo 22 zimebainishwa. Msisitizo mkubwa utawekwa katika kuimarisha mfumo wa kitaasisi; kuweka mazingira ya kuvutia shughuli za kibiashara; kubainisha majukumu ya serikali na sekta binafsi; uuzaji na ununuzi wa mazao na pembejeo na kuhuisha mipango ya maendeleo ya kilimo katika sekta nyingine. Lengo ni kuongeza tija na faida katika kilimo.

- Kuoanisha Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini ili kutatua vikwazo vya uzalishaji ambavyo vimedidimiza maendeleo ya sekta ya kilimo kama vile barabara zisizopitika nyakati za masika, uharibifu wa mazingira na athari za ukimwi.

- Kuwiainisha kodi na ushuru unaotozwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwenye mazao mbali mbali ili kupunguza idadi za kodi na kumwezesha mkulima na mfugaji kupata bei nzuri na hivyo kuinua kipato chake.

- Kushirikiana na wahisani ili kutekeleza miradi midogo midogo na ya asili ya umwagiliaji nchini kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula.

37. **Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na matukio ya hali ya ukame unaotokea mara kwa mara nchini serikali ikishirikiana na serikali ya Japan tangu mwaka jana (Novemba, 2001) imeanza kuandaa mpango kamambe wa kuendeleza

kilimo cha umwagiliaji nchini (National Irrigation Master Plan). Awamu ya kwanza ya maandalizi ya mpango huu itakamilika mwezi Oktoba, 2002. Mpango huu utazingatia: umuhimu wa kuweka uwiano wa matumizi bora ya maji na ardhi na kutumia gharama nafuu anazoweza kuzimudu mkulima mdogo; kubainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo kwa nchi nzima; ukusanyaji wa takwimu na kubaini fursa na maeneo maalum ambayo yatawaelekeza wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji. Ni matumaini yangu kwamba mpango huu utawavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta ya kilimo.

38. **Mheshimiwa Spika,** wakulima na wawekezaji wadogo wadogo wanaowekeza katika shughuli zenye uhusiano na sekta ya kilimo ndio kwa kiwango kikubwa wameathirika kutokana na kukosekana kwa fursa ya kupata mikopo yenye riba nafuu kutoka katika mabenki yaliyoko nchini. Ili kuondokana na hali hii, Serikali katika mwaka 2001 iliendelea kuhimiza uanzishwaji wa benki za maendeleo ya jamii (Community banks) zitakazotoa huduma ya mikopo midogo midogo hasa kwa wakulima. Aghalabu, benki kadhaa zimeanza kutoa huduma hiyo zikiwemo Kilimanjaro Cooperative Bank, Mufindi Community Bank, Akiba Commercial Bank, CRDB Bank Ltd., NMB na Tanzania Postal Bank na Dar-es-Salaam Cooperative Bank. Vile vile, katika ngazi ya vijiji na jumuiya baadhi ya vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa vimeanza kuimarika na kuonyesha mafanikio ya kuridhisha. Serikali pia, itaendelea kuhimiza utekelezaji wa sera ya mikopo midogo (Microfinancing Policy) ili huduma ya mikopo ipatikane kwa wakopaji wadogo wadogo hasa wakulima.

Sekta ya Viwanda

39. **Mheshimiwa Spika**, serikali iliendelea kutekeleza sera yake ya kufufua viwanda, kurekebisha uchumi, na kutafuta masoko. Kutokana na juhudi hizo ukuaji wa sekta uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2001 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2000. Sekta pia iliongoza kuwavutia wawekezaji wengi zaidi ikilinganishwa na sekta nyingine ambapo karibu asilimia 46 ya miradi yote ya sekta binafsi iliwekezwa kwenye uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Sheria ya kuanzisha EPZ ilipitishwa na Bunge na Tanzania ilikamilisha taratibu za kujiunga na kutumia fursa ya kuuza mazao nje chini ya mpango wa “AGOA” ambapo chini ya mpango huu, tayari baadhi ya viwanda vimefaidika kwa kuuza bidhaa nje zenye thamani ya dola 1.0 milioni.

Sekta ya Madini

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2001, ukuaji wa sekta ya madini ulifikia asilimia 13.5 ikilinganishwa na asilimia 13.9 mwaka 2000. Kushuka kwa ukuaji kulitokana na kupungua kwa kiasi cha uzalishaji na mauzo kwa baadhi ya madini ya vito vya thamani. Hata hivyo, thamani ya mauzo nje ya bidhaa za madini yalikuwa ya kuridhisha ambapo jumla ya dola 311 milioni zilipatikana mwaka 2001 ikilinganishwa na jumla ya dola 185 milioni zilizopatikana mwaka 2000, sawa na ongezeko la asilimia 69. Ongezeko hili lilitokana zaidi na mauzo ya dhahabu na almasi.

41. **Mheshimiwa Spika**, uwekezaji kwenye sekta ya madini mwaka 2001 ulikuwa dola 1,307.6 milioni ambapo zaidi ya asilimia 90 iliwekezwa kwenye madini ya dhahabu. Aidha, utafutaji wa madini hasa dhahabu, almasi, vito vya thamani uliendelea kufanywa katika Wilaya ya Nzega, Kahama, Geita, Handeni, Tarime, Musoma, Simanjiro, Shinyanga, Ludewa, Chunya, Ngara na Mbeya. Ni nia ya serikali kuendelea kukuza uhusiano mzuri kati ya wenyeji waliopo katika maeneo ya migodi mbalimbali nchini na makampuni yanayochimba madini. Serikali pia itahimiza makampuni husika ya madini kuchangia katika shughuli za maendeleo katika maeneo yanayozunguka migodi.

Sekta ya Biashara

42. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2001 ukuaji wa sekta ya uuzaji jumla, rejareja na mahoteli ikijumuisha utalii ilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2000. Mambo yaliyofanyika ni pamoja na:- uratibu na uhuishaji wa sera na sheria za utalii; ushiriki kwenye maonyesho na kutangaza vivutio vilivyopo na maeneo ya uwekezaji; na ukamilishaji wa maandalizi ya vigezo vitakavyotumika kuziweka hoteli katika madaraja ili kudhibiti huduma zitolewazo; na udhibiti wa mapato ya utalii.

MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

43. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2001/02 serikali iliendelea kutekeleza program ya kuboresha barabara na mawasiliano ambayo inalenga katika kuimarisha mtandao mzuri wa barabara, madaraja na vivuko ili zipate kupitika nyakati zote kama kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi. Hadi kufikia Desemba 2001, Serikali ikishirikiana na wananchi imefanikiwa kutengeneza kilometa 2,063 za barabara kuu na kilometa 1,683 za barabara vijijini. Aidha,

ujenzi wa daraja la Mto Rufiji unaendelea vizuri na linategemewa kufunguliwa kati ya Agosti na Septemba 2002.

44. **Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika kuchochea maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii na katika uzalishaji mali ni mkubwa. Katika mwaka 2001, sekta ya mawasiliano na uchukuzi ilikua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.1 mwaka 2000. Ukuaji huu ni matokeo ya ushirikishwaji madhubuti wa sekta binafsi ambayo kwa sasa inatoa huduma hii kwa ushindani mkali. Aidha, kuongezeka kwa uwekezaji katika mawasiliano kwa njia ya simu na usafiri wa anga, barabara na maji nako kulichangia katika ongezeko hili.

Sekta ya Nishati

45. **Mheshimiwa Spika**, serikali inaendelea na juhudi zake za kuendeleza sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti za nishati nafuu ili kukidhi mahitaji ya nishati kwa sekta zote hususan za uzalishaji mali kwa lengo la kupunguza matumizi ya mafuta na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji miti. Aidha, mwezi Oktoba, 2001 serikali, Benki ya Dunia na wahisani wengine walikamilisha makubaliano ya uendelezaji wa mradi wa gesi wa Songo Songo na utekelezaji wake utaanza mwaka 2002/03 na utakamilika mwaka 2004.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuendeleza sekta ya nishati nchini, serikali imedhamiria kuendeleza mradi wa Mchuchuma ambao unajumuisha miradi yenye uwiano na kutegemeana ya ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka Mchuchuma hadi Mufindi na kuunganisha katika gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huu unakwenda sambamba na uendelezaji wa ukanda wa maendeleo ya Mtwara na ile ya Mingoyo hadi Mbamba-Bay pamoja na ujenzi/upanuzi wa bandari za Mtwara na Mbamba-Bay. Mradi huu ni muhimu kitaifa na unatarajiwa kukidhi mahitaji halisi ya umeme kwa sekta mbali mbali nchini na zaidi sana kusaidia kuondoa tatizo la nishati kwenye mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Lindi na Rukwa.

HUDUMA ZA KIJAMII

Sekta ya Elimu.

47. **Mheshimiwa Spika,** maendeleo ya sekta ya elimu kwa jumla yalijionyesha katika kupanuka na kuboreka kwa elimu ya awali, msingi na sekondari. Mathalani katika kipindi cha 2001/02, mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi (PEDP) ulianza kutekelezwa kwa kufuta michango ya UPE ya sh. 2,000 kwa kila mwanafunzi. Aidha, serikali ilitoa fedha (Capitation Grant) sh. 9,000 za uendeshaji wa shule kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi. Serikali pia ilitoa fedha za ujenzi wa madarasa (Development Grant) ili kuinua ubora wa elimu ya msingi. Mipango hii imelenga katika kutumia jumla ya sh. 281,540.4 milioni. Kiasi cha sh. 232,296.9 milioni zimekwishatolewa kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini. Jitihada pia zilifanywa na serikali na sekta binafsi za kuimarisha na kupanua elimu ya ufundi na elimu ya juu.

48. **Mheshimiwa Spika,** ongezeko katika bajeti na marekebisho mengine katika mifumo ya ada yamechangia katika ongezeko la uandikishaji katika shule za msingi. Mathalani, katika mwaka 2001 idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi ilifikia watoto 1,558,000 ambayo ni zaidi ya lengo lililowekwa la kuandikisha watoto 1,500,000. Aidha, idadi ya watoto wote walioko katika elimu ya msingi kutoka darasa la kwanza hadi la saba (I – VII) wenye umri wa kati ya miaka 7 hadi 13 ilifikia watoto 5.9 milioni ambayo ni zaidi kuliko idadi ya watoto 4.8 milioni waliotarajiwa mwanzoni. Pia, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari na elimu ya juu. Aidha, kumekuwepo na maendeleo katika upanuzi wa elimu ya awali kwa mwaka 2001. Ongezeko hilo limetokana na utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 iliyoagiza kila shule ya msingi iwe na darasa la elimu ya awali, hivyo wazazi na taasisi mbalimbali wamehamasika kuanzisha madarasa ya elimu ya awali. Pia, mpango wa kugharamia elimu kwa wanafunzi wa kike wanaosoma sekondari (GSES) ambao wazazi wao hawana uwezo umesaidia wanafunzi wengi zaidi. Sekta binafsi imechangia katika maendeleo ya elimu kwa ngazi zote, ikiwa na wanafunzi 333,971 katika elimu ya awali, ukilinganisha na wanafunzi 581,022 katika shule za serikali. Kwa upande wa elimu ya sekondari sekta ya binafsi ilikuwa na shule 491 kati ya shule 979 zilipo za sekondari, vyuo vya elimu ya ufundi zaidi ya 600 na vyuo vikuu 7 kati ya 11 vilivyoko nchini.

Sekta ya Afya

49. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya afya, kwa mwaka 2001, serikali iliendelea kutekeleza programu ya kuboresha sekta ya afya ambayo inalenga katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya na uboreshaji wa afya ya misingi kwa wananchi wote. Matokeo ya utekelezaji yamekuwa ya kuridhisha. Upatikanaji wa madawa umekuwa bora zaidi, idadi ya watoto waliopatiwa chanjo dhidi ya surua, kifaduro, polio na pepopunda imeongezeka na kampeni dhidi ya Ukimwi imewaelimisha watu wengi na wametambua kwamba ukimwi ni hatari na ni janga la Taifa. Kwa jumla magonjwa ya malaria, kuhara, kuhara damu na magonjwa ya koo (ARI) yameendelea kuongoza katika kuathiri watu wengi zaidi, hii ikiwa ni pamoja na ukimwi.

Sekta ya Maji

50. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2001, serikali iliendelea kuifanyia mapitio sera ya maji na uondoaji majitaka ili kuweka mazingira mazuri ya kuishirikisha

sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji nchini. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha mamlaka za maji mijini kwa kuunda muundo wa mamlaka za daraja la B na C na kuzipatia watumishi pamoja na vitendea kazi. Sera ya maji inalenga pia katika kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya vyanzo vyote vya maji nchini ikiwa ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

MASUALA MENGINEYO YA KITAIFA

Idadi ya Watu na Maendeleo

51. **Mheshimiwa Spika,** idadi ya watu waishio Tanzania imeendelea kuongezeka kwa kiwango kile kile cha asilimia 2.8 kwa mwaka na hivyo kufanya hesabu yao (makadirio) kufikia watu 33,857,356 ilipofikia mwaka 2001. Kwa ukuaji huu wa idadi ya wakazi uchumi nao ulitakiwa ukue kwa kiwango kuanzia asilimia 7 na kuendelea kwa mwaka ili kumudu kutimiza mahitaji ya maendeleo ya watu hao. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba ukuaji wa uchumi wa asilimi 5.6 uliofikiwa mwaka 2001 ulikuwa bado ni wa kiwango kidogo mno kisichowezesha kufanya maendeleo makubwa. Tatizo la wakimbizi kutoka nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Rwanda liliendelea na kuchangia katika ongezeko la idadi ya watu nchini.

Watoto wenye umri chini ya miaka 15 na vijana wa rika la miaka 15 – 24 kwa pamoja waliendelea kuwa ndiyo sehemu kubwa (zaidi ya asilimia 50) ya watu wote waliopo. Hali hii kwa pamoja inabainisha kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za elimu, afya, maji, ajira na kadhalika.

52. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hali hiyo jitihada za kuboresha hali ya maisha ya watu ziliendelea. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (Country Population Programme) ambapo mpango wa nne wa miaka mitano (1996–2001) ulifungwa na kufuatiwa na mwingine wa (2002–2006) ulioandaliwa katika mwaka 2001. Mipango yote hii inalenga katika:

- Kuboresha na kupanua huduma na afya ya uzazi ikiwemo uzazi wa mpango.
- Kuimarisha usimamiaji na utekelezaji wa sera ya taifa ya idadi ya watu
- Kukuza dhana ya idadi ya watu na maendeleo na kuzingatia masuala ya jinsia kama sehemu muhimu ya masuala ya idadi ya watu.

MKAKATI WA TAIFA WA KUPUNGUZA UMASKINI

53. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya msingi yaliyopatikana katika kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini yamebainishwa katika taarifa ya utekelezaji wa mkakati huo kwa mwaka 2000/01. Matokeo ya mipango iliyobuniwa ni pamoja na kuboresha uchumi kwa jumla ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Hata hivyo, sekta ya kilimo haijafikia kukua kwa kiwango cha juu kinachohitajika ili kuondoa umasikini. Kwa maeneo mengine, muda wa utekelezaji uliopita ni mfupi kuweza kupima mafanikio yaliyopatikana. Hata hivyo, kumekuwepo na mafanikio yanayotia matumaini hasa kwa upande wa elimu (hususan kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi); afya (kupanuka kwa udhibiti wa magonjwa ya watoto na uimarishaji wa huduma za uzazi); uwezeshaji wa wananchi kujipatia mikopo midogo kwa shughuli za kiuchumi; na kuendeleza marekebisho ya serikali za mitaa na utendaji katika ngazi za vijiji.

Kudhibiti kuenea kwa Ukimwi

54. **Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imeendelea kukabiliwa na janga kubwa la ukimwi na hivyo kuwa ni mzigo mkubwa kwa uchumi wetu kwa maana ya kuongezeka kwa gharama za matibabu na watu wengi kushindwa kuhudhuria katika kazi za uzalishaji. Wataalamu wengi wanakufa wakiwa bado katika umri wa kufanya kazi. Kwa hakika janga hili limeendelea kusababisha kupungua kwa tija katika uzalishaji, kupungua kwa umri wa wastani wa kuishi, kuongezeka kwa uwiano wa watu tegemezi na pia kuathiri matarajio ya ukuaji wa uchumi. Idadi kubwa ya watu wanaoambukizwa na kuathirika na ugonjwa wa ukimwi imeendelea kuwa ni vijana wa rika kati ya miaka 15 hadi 49 na wanawake wakiwa ndio walio wengi. Kwa mfano wa upande wa Tanzania Bara takwimu zinaonyesha kwamba karibu asilimia 11 ya walioambukizwa walikuwa ni watu katika rika hilo la miaka kati ya 15 hadi 49 wakati asilimia 60 ya maambukizi mapya yalitokea kwa watu wa rika kati ya miaka 15 hadi 24.

55. **Mheshimiwa Spika,** juhudi za kitaifa na kimataifa zimeendelea ili kukabiliana na janga hilo la ukimwi pamoja na athari zake mbali mbali. Serikali imeendelea kushirikiana na wadau wengine katika nyanja mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa sera ya kudhibiti ukimwi, na kuundwa kwa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ambayo imepewa jukumu la kuratibu jitihada zote za

kupambana na ukimwi. Aidha, kampeni dhidi ya ukimwi imefanyika nchini pote; jambo ambalo limefungua fursa mpya ya kupambana na ukimwi katika ngazi zote.

Jinsia

56. **Mheshimiwa Spika,** mchango mkubwa unaotolewa na wanawake katika kuendeleza taifa letu sote tunauelewa. Kwa mwaka 2001/02 serikali imeendelea na juhudi zake za kuhakikisha kwamba masuala ya jinsia yanazingatiwa kikamilifu katika mfumo wa utayarishaji na utekelezaji wa mipango na bajeti na katika usimamizi wa uchumi katika ngazi na nyanja zote. Kwa mwaka 2001/02 serikali ikishirikiana na taasisi inayoshughulikia mtandao wa jinsia nchini (Tanzania Gender Networking Programme) iliendelea na juhudi zifuatazo: Kukamilisha na kuhuisha sera ya jinsia; Kuanzisha vitengo vya kushughulikia masuala ya jinsia katika taasisi za umma; Kufanya maandalizi ya awali ya uanzishaji wa benki za wanawake; Kutayarisha program itakayorahisisha kutungamanisha masuala ya jinsia katika kuendeleza kilimo na kuendeleza mafunzo ili kuinua viwango vya elimu ya wanawake na kujenga kujiamini zaidi kwa wanawake walio katika ngazi za uongozi. Lengo la jitihada hizo ni kuboresha mahusiano kati ya jinsia zote na kuinua usawa, haki na maendeleo kwa watu wote.

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2002/03 serikali kwa kushirikiana na taasisi zingine itaendelea kutoa mafunzo kwa mikoa na serikali za mitaa kwa nia ya kujenga uwezo wa maafisa mipango katika kubuni kutayarisha, kutekeleza, kudhibiti na kutathmini mipango ya maendeleo na bajeti inayozingatia masuala ya jinsia. Aidha, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ikishirikiana na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na taasisi inayoshughulikia mtandao wa jinsia nchini (TGNP) itatayarisha kijitabu kinachotoa mwongozo wa kutayarisha mipango na maendeleo na bajeti inayotungamanisha masuala ya jinsia katika ngazi ya wilaya, kata na kijiji.

Nguvu kazi na Ajira

58. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utafiti wa nguvu kazi uliofanyika mwaka 2000/2001 yanaonyesha kuwa kati ya mwaka 1990/91 na 2000/01 nguvukazi imekuwa ikiongezeka kwa zaidi ya watu 650,000 kila mwaka. Katika mwaka 2001 nguvukazi ilifikia watu milioni 17.8, kati ya hao, walioajiriwa kwa tafsiri ya Tanzania walikuwa milioni 15.5. Nguvukazi iliyokuwa haina ajira ilikuwa milioni

2.3 kwa nchi nzima, sawa na asilimia 12.9 ya nguvukazi yote. Matokeo ya utafiti huo pia yanabainisha kuwa ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa kwa vijana wengi wanaoingia katika soko la ajira kwa mara ya kwanza. Tatizo hilo likitazamwa kijinsia linaonekana kuwaathiri zaidi vijana wa kike kuliko wa kiume.

59. **Mheshimiwa Spika,** serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo la ajira ikiwa ni pamoja na kuanzisha mifuko ya kujitegemea kwa wanawake, vijana na wafanyabiashara wadogo wadogo kwa nia ya kuwapa mikopo ya masharti nafuu. Aidha, mashirika yasiyo ya kiserikali ya hapa nchini na ya nje yamekuwa yakihamasishwa na kuhimizwa na serikali ili yaweze kuchangia katika kupambana na tatizo la ajira. Vile vile, sera ya taifa ya ajira ya mwaka 1997 imehuishwa kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii yaliyotokea katika kipindi hiki.

60. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2002/2003 serikali itaongeza juhudi zake za kukabiliana na tatizo la ajira kwa kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji kutoka nje na ndani ili waweze kuwekeza na hivyo kuongeza nafasi za ajira. Pia serikali itahimiza uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza ajira. Aidha, vyuo vya majaribio ya ufundi vitahimizwa kutoa mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

SENSA YA WATU NA MAKAZI MWEZI AGOSTI 2002

61. **Mheshimiwa Spika**, sensa ya watu na makazi ilifanyika mara ya mwisho mwezi Agosti 1988 na sasa itafanyika tarehe 25 Agosti 2002. Maandalizi muhimu yamekwishakamilika. Ili kufanikisha sensa, shule zote za msingi zitafungwa mwanzoni mwa mwezi Agosti mwanzoni hadi katikati ya mwezi Septemba ili kuwawezesha walimu wa shule hizo kushiriki kikamilifu katika kazi ya kuhesabu watu. Nachukua nafasi hii kuwashukuru Wahisani hususan UNFPA, DFID na Sweden kwa msaada wao unaofanikisha zoezi hili.

MATARAJIO KWA MWAKA 2002/03

Shabaha ya Jumla ya Uchumi

62. **Mheshimiwa Spika**, Shabaha na mwelekeo wa mpango na bajeti ya mwaka 2002/03 umezingatia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mkakati wa Kupunguza Umaskini; Ukamilishaji wa masharti ya kusamehewa madeni

(HIPC Completion Point); mwenendo wa uchumi wa bajeti katika mwaka 2001/02; na masuala ya kisera yaliyojitokeza. Kwa kuzingatia mtazamo huo malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii katika mwaka 2002/03 yatakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa halisi kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2002 na asilimia 6.3 mwaka 2003;

(ii) Kuwa na kiwango cha kasi ya upandaji bei kisichozidi asilimia 4.2 ifikapo Juni 2003;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani ya serikali kwa uwiano wa Pato la Taifa wa asilimia 12.5 mwaka 2002/03;

(iv) Kudhibiti ujazi wa fedha (M_2) kwa viwango vinavyowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kupungua kwa kasi ya upandaji bei; na

(v) Kuongeza akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa huduma na bidhaa toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

MASUALA YA KUZINGATIA KATIKA KUTEKELEZA MALENGO YA MPANGO WA MUDA WA KATI NA BAJETI

Kufufua dhana ya Kujitegemea

63. **Mheshimiwa Spika,** baada ya dalili za kutengemaa kwa uchumi kuonekana, kazi kubwa iliyo mbele yetu kama Taifa ni kuingiza ndani ya fikra zetu dhana ya ukuzaji wa uchumi ili tuanze kuelekea kwenye hatua ya kuongeza uwingi na ubora wa bidhaa zetu zinazozalishwa nchini. Ili Pato halisi la Taifa lipate kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2003 na asilimia 7.0 mwaka 2004, pamoja na masuala mengine Watanzania tunahitaji kujijengea utamaduni na fikra sahihi za kuthamini kazi kama ndio msingi wa kujiletea maendeleo. Sasa muda umefika wa kujenga fikra za kujitegemea na kuwa na uchungu wa utegemezi na kupokea misaada ambayo inaweza kutudhalilisha. Aidha, waheshimiwa wabunge kama wawakilishi wa watu na watumishi wa umma hatuna budi kuelewa na kuhamasishana kwa nguvu juu ya azma ya watanzania ya kujenga msimamo sahihi wa kubadilisha mtazamo na kujenga fikra ili kwenda sambamba na mabadiliko ya haraka ya kiuchumi yanayotokea hivi sasa duniani. Kama Taifa tunahitaji sasa kuanzisha na kuhamasisha kampeni maalum ya *kukuza uchumi* wetu miongoni mwa Watanzania (to instill economic growth), ili kuondokana na umaskini.

64. **Mheshimiwa Spika,** ili nchi yetu iondokane na bajeti tegemezi, umaskini uliokithiri, ukosefu wa ajira kwa vijana wetu na miundombinu hafifu hatuna budi kutoa kipaumbele na mihadi katika kutekeleza kwa bidii zote haya yafuatayo:-

- **Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo**. Kwa kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa kwa sekta hii zinaelekezwa katika maeneo yatakayoongeza uwezo wetu katika kuzalisha mazao mbali mbali ya asilia na yasiyo ya asilia.

- **Kutekeleza Mkakati wa Maendeleo Vijijini**. Katika kutekeleza mkakati huu tuelekeze nguvu zetu katika kukwamua maeneo ambayo ni vikwazo katika kuimarisha uchumi vijijini. Maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele ni kama vile ubovu wa barabara, udhaifu wa taratibu za masoko kwa mazao ya wakulima, upungufu wa huduma za hifadhi na upatikanaji wa kuaminika wa zana na pembejeo za kilimo n.k.

- **Kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini**. Mkakati huu unaojielekeza katika kuboresha elimu, afya, maji, barabara vijijini na ukuzaji wa ajira na mapato huko vijijini tayari umeshatengewa fedha zake hasa katika sekta ya elimu. Sote kwa pamoja tuhakikishe kuwa fedha hizo zinawanufaisha walengwa na zinatumika kwa malengo yaliyopangwa. Utaratibu huu utahakikisha kuwa mafanikio ya ukuaji wa uchumi yanawafikia wananchi wa kawaida.

- **Kuongezea wakulima uwezo kifedha.** Serikali kupitia kanuni na taratibu za fedha ihakikishe kuwa wakulima wadogo wanapunguziwa kodi kwa kiwango kikubwa ili waweze kuinua uwezo wao wa kununua (i.e. *purchasing power),* uwezo wao wa kimapato na viwango vya motisha katika uzalishaji. Utaratibu wa kuoanisha kodi na matozo ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu itasaidia sana kuibua viwango vya uzalishaji vijijini.

- **Kuongeza uzalishaji ili kukuza ukuaji wa Pato la Taifa.** Ili kukuza uzalishaji kwa nia ya kuondokana na tatizo la kasi ndogo ya kukua kwa Pato la Taifa hapana budi kuelekeza nguvu zetu katika maeneo yatakayoibua uchumi. Tunaweza kufikia lengo hili kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kama vile pamba, korosho, kahawa, katani n.k.; kurekebisha viwanda husika na mikoa, kuwavutia wawekezaji katika maeneo haya kwa nguvu zaidi kwa kujitangaza kwa njia ya kuandaa *Regional Investment Profiles* na kuziwasilisha TIC.

(ii) Kukazania uanzishaji wa viwanda vidogo na vya kati vinavyosindika mazao ili tupate kukuza ajira na kuongeza thamani ya bidhaa tunazozalisha nchini.

(iii) Serikali kuendeleza jitihada zake za kuboresha na kuwapatia wananchi wenye vipato vya chini fursa ya kupata mikopo kupitia benki za jumuiya na benki zingine zilizoko nchini. Aidha, suala la riba halina budi kutazamwa upya ili kuhakikisha kwamba viwango vya riba katika mabenki vinapungua ili kuwezesha watu wengi zaidi kutoka sekta binafsi kupata mikopo na kuwekeza katika kukuza uchumi.

(iv) Kujenga nidhamu na uwajibikaji wa hali ya juu katika matumizi ya fedha ili zipate kutuletea maendeleo yanayokusudiwa.

(v) Kuendeleza kwa nguvu zote zoezi lililopo la kurekebisha na kukodisha/kubinafsisha mashirika yetu kwa kuwashirikisha na kuwaelimisha wafanyakazi husika kila hatua zinavyoendelea katika zoezi hili ili waelewe na kuwa tayari kwa mabadiliko.

MAJUMUISHO

65. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuelezea matarajio na misingi hiyo hapo juu, mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo yetu kwa mwaka 2001 yanaonyesha wazi kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa njia ya kutayarisha na kutekeleza sera, mikakati na programu mbali mbali za mageuzi kwa kiasi zimeanza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Mafanikio tuliyopata ni pamoja na kufanya vizuri katika vigezo vya Uchumi Jumla (*macro economy*). Hata hivyo, kama watanzania bado tunayo kazi na changamoto kubwa.

Kwanza ni jinsi gani uimara huu wa Uchumi Jumla tulioujenga utakuwa endelevu ili tusije tukatetereka tena. **Pili** utengemavu na utulivu wa Uchumi

Jumla (*macro economic Stability*) ni sharti la lazima lakini halitoshelezi masharti na azma yetu ya kupunguza umaskini. Swali la msingi ni jinsi gani mafanikio ya Uchumi Jumla yatanufaisha wananchi wa kawaida kuondokana na umaskini vijijini na mijini. Aidha, sote kwa pamoja tutafuatiliaje ili kuhakikisha kuwa mipango na rasilimali zinazotengwa kwa mikakati ya kupunguza umaskini zinawafikia walengwa husika? Kazi hii ni ya sote watanzania na tutafanikiwa ikiwa kwa dhati kila mmoja atatimiza wajibu wake.

66. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia. Ninapenda nizitaje baadhi ya nchi na Mashirika ya kimataifa yafuatayo: Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani (IMF) Mashirika mbali mbali ya Umoja wa Mataifa kama vile UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD, WFP na WHO, Jumuiya ya nchi za Ulaya, mfuko wa fedha wa nchi wanachama wa uzalishaji mafuta (OPEC Fund), Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA), Shirika la Maendeleo la Finland (FINNIDA), Shirika la Maendeleo la Kanada (CIDA), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Serikali ya Uswizi, Uholanzi, serikali ya Ujerumani, Shirika la Maendeleo la Japan, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Afrika ya Kusini, Kuwait, Italia, Ireland na nchi zingine marafiki na mashirika mbali mbali ya Kimataifa yasiyo ya kiserikali (NGO's). Wote hawa wametoa mchango mkubwa sana katika maendeleo yetu.

67. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja

Jedwali Na.1: Mwenendo kwa Baadhi ya Vigezo vya Kiuchumi

Na.	KIASHIRIO	1995	1996	1997	1998	1999	2000	2001
1	Wastani wa Pato kwa kila mtu	101696.1	121998.5	147134.0	170843.7	193453.0	208892.9	231426.0
2	Uwekezaji wa mitaji (% ya Pato la Taifa)	21.5	18.2	16.3	17.6	19.9	20.3	20.4
3	Mfumuko wa bei	27.4	21.0	16.1	12.9	7.8	6.0	5.2
4	Urari wa kawaida (% Pato la Taifa) kwa miaka husika	12.7	8.0	8.1	13.2	10.6	4.6	5.0
5	Kiwango wastani cha kubadilisha Sh/dola	550.4	595.6	624.6	664.7	748.1	800.7	917.4
		1994/95	1995/96	1996/97	1997/98	1998/99	1999/2000	2000/01
6	Naksi ya bajeti kabla ya ruzuku (% Pato la Taifa	-3.1	0.1	-0.7	-2.3	-2.3	-4.5	-4.9
7	Wastani wa riba za amana za akiba	15.0	12.0	12.8	12.0	7.4	7.1	4.1
8	Wastani wa riba za mikopo ya muda mfupi	31.0	28.0	24.5	28.0	21.4	19.1	20.9
9	Malipo ya deni la nje (% mauzo ya nje)	16.5	17.3	17.5	18.4	17.4	15.8	10.2
10	Malipo ya deni la nje (% Pato la Taifa)	7.2	8.8	9.4	9.0	9.0	5.6	1.7
11	Madeni ya Ndani (% Pato la Taifa)	-	-	22.3	18.4	16.0	14.5	10.7

Chanzo: Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

Jedwali Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa Halisi Kisekta

Na.	Aina ya Sekta	1996	1997	1998	1999	2000	2001
1.	Kilimo	3.9	2.4	1.9	4.1	3.4	5.5
2.	Uchimbaji wa Madini na Mawe	9.6	17.1	27.4	9.1	13.9	13.5
3.	Bidhaa za viwandani	4.8	5.0	8.0	3.6	4.8	5.0
4.	Umeme na Maji	11.1	2.2	5.5	3.9	5.9	3.0
5.	Ujenzi	7.6	8.2	9.9	8.7	8.4	6.7
6.	Biashara, uuzaji jumla, rejareja na mahoteli	3.5	5.0	4.7	6.0	6.5	6.7
7.	Mawasiliano na Uchukuzi	1.1	4.9	6.2	5.8	6.1	6.3
8.	Fedha, Bima na Huduma za Kibiashara	0.4	7.7	5.6	4.1	4.7	3.3
9.	Uendeshaji Serikali na Huduma nyingine	1.6	3.2	2.7	3.5	3.6	3.5
10.	Ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka unaohusika.	4.2	3.3	4.0	4.7	4.9	5.6
11.	Mwaka wa Fedha	1995/96	1996/97	1997/98	1998/99	1999/2000	2000/01
12.	Ukuaji wa Pato la Taifa --kwa Mwaka wa Fedha.	3.9	3.7	3.7	4.4	4.8	5.3

Chanzo: Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

Jedwali Na. 3: Mauzo Nje ya Bidhaa na Huduma 1996-2001 (Milioni dola za Kimarekani)

BIDHAA	1996	1997	1998	1999	2000	2001	BADILIKO (%)
Bidhaa Asilia							
Kahawa	136.11	119.28	108.74	76.60	83.70	57.10	-31.78
Pamba	125.33	130.38	47.63	28.50	38.00	33.70	-11.32
Katani	5.32	9.12	6.78	7.30	5.60	6.70	19.64
Chai	22.54	31.83	30.43	24.60	32.70	29.00	-11.31
Tumbaku	49.24	53.64	55.39	43.40	38.40	35.70	-7.03
Korosho	97.77	91.08	107.32	100.90	84.40	56.60	-32.94
Karafuu	-	-	-	19.90	10.0	12.30	23.00
Jumla ndogo ya bidhaa asilia	**436.31**	**435.33**	**356.29**	**301.20**	**292.80**	**231.10**	-21.07
Bidhaa zisizo Asilia:							
Bidhaa za Petroli	15.79	7.12	0.10	0.40	0.10	0.00	0.00
Madini	55.85	51.08	26.37	73.30	185.10	302.20	63.26
Bidhaa za viwandani zilizosindikwa*	122.80	111.33	35.69	30.10	43.40	56.20	29.03
Samaki na bidhaa zake		56.34	74.28	56.69	76.30	96.80	29.26
Mazao ya Mboga na Maua		5.23	8.64	8.88	9.70	11.00	13.4
Bidhaa zinginezo		86.13	87.16	92.18	54.80	79.20	44.53
Jumla ndogo ya bidhaa zisizo asilia	**327.45**	**317.22**	**232.24**	**270.45**	**369.40**	**545.40**	**47.25**
Jumla ya Mauzo ya Bidhaa		**752.55**	**588.53**	**571.63**	**663.20**	**776.50**	**15.58**
Mapato kutokana na Huduma mbalimbali		493.93	553.00	646.40	666.70	712.40	7.64
Jumla ya Mauzo Nje ya Bidhaa na Huduma		**1,246.38**	**1,141.52**	**1,218.03**	**1,333.90**	**1,488.90**	10.86

Chanzo: Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji; Benki Kuu ya Tanzania

* Bidhaa zilizosindikwa: Nyuzi za Pamba, Kahawa, Tumbaku, mazao ya Katani, n.k.

Jedwali Na. 4: Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

	1996 (Halisi)	1997 (Halisi)	1998 (Halisi)	1999 (Halisi)	2000 (Halisi)	2001* (Matarajio)
Urari wa Biashara	**-448.8**	**-395.4**	**-777.5**	**-824.9**	**-671.7**	**-713.3**
Bidhaa zilizouzwa	763.8	752.6	588.5	543.3	663.2	776.4
Bidhaa zilizonunuliwa	1,212.6	1,148.0	1,366.0	1,68.2	1,334.9	1,489.7
Urari wa Huduma	-278.8	-306.4	-441.1	-226.8	-92.8	-98.9
Mapato	537.1	493.8	553.0	646.4	666.7	712.4
Malipo	815.9	800.2	994.1	873.2	759.5	811.3
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-72.0	-122.8	-124.5	-75.4	-83.3	-44.1
Yaliyoingia	41.5	44.9	48.0	56.1	60.0	82.0
Yaliyotoka	113.5	167.7	172.5	131.5	143.3	126.1
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	**338.4**	**266.0**	**350.0**	**333.7**	**465.8**	**442.8**
Iliyoingia	370.7	333.7	376.9	457.0	542.6	516.6
Serikalini	236.0	235.3	260.6	295.2	448.0	409.6
Sekta nyingine	134.7	98.4	116.3	161.8	94.6	107.0
Iliyotoka	32.3	67.7	26.9	123.3	76.8	73.8
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	**-461.2**	**-558.6**	**-993.1**	**-793.4**	**-382.0**	**-413.5**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	191.0	166.9	299.5	322.5	330.4	382.6
Iliyoingia	191.0	166.9	299.5	322.5	330.4	382.6
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0

Urari katika uwekezaji	0.3	-139.9	14.4	177.2	162.3	6.4
Uwekezaji wa miradi	148.5	157.8	172.2	183.4	192.8	224.8
Uwekezaji katika hisa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Uwekezaji aina nyingine	-148.2	-297.7	-157.8	-6.7	-30.5	-218.4
Makosa na Masahihisho	38.8	-101.8	33.2	-79.0	-146.2	79.5
Urari wa malipo yote	**-231.2**	**-633.4**	**-646.0**	**-372.7**	**-35.5**	**55.0**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*: Ya muda

Jedwali Na. 5: Malengo ya Ukuaji wa Pato la Taifa Halisi Kisekta 2000-2005 (Kwa Bei za Mwaka 1992)

Na.	Aina ya Sekta	2000	2001	2002	2003	2004	2005
1.	Kilimo	3.4	5.5	5.3	5.4	5.5	5.5
2.	Uchimbaji wa Madini na Mawe	13.9	13.5	12.1	11.0	10.5	10.3
3.	Bidhaa za viwandani	4.8	5.0	6.2	6.6	7.0	7.7
4.	Umeme na Maji	5.9	3.0	5.1	5.3	5.6	5.8
5.	Ujenzi	8.4	6.7	6.2	5.5	5.6	5.7
6.	Biashara, uuzaji jumla, rejareja na mahoteli	6.5	6.7	7.9	8.1	8.4	8.7
7.	Mawasiliano na Uchukuzi	6.1	6.3	7.7	8.3	8.8	9.2
8.	Fedha, Bima na Huduma za Kibiashara	4.7	3.3	5.2	5.3	5.7	6.6
9.	Uendeshaji Serikali na Huduma nyingine	3.6	3.5	3.9	4.5	5.3	5.5
10.	Ukuaji wa Pato la Taifa --Mwaka husika.	4.9	5.6	5.9	6.3	6.6	7.0
11.	Mwaka wa Fedha	1999/2000	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05
12.	Ukuaji wa Pato la Taifa --Mwaka Fedha.	4.8	5.3	5.8	6.1	6.5	6.8

Chanzo: Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji